

# **HALMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA**



## **TANGAZO LA ZABUNI**

### **ZABUNI YA UPANGAJI WA VYUMBA VYA BIASHARA**

1. Halmashauri ya Jiji la Arusha inakusudia kupata wapangaji watakaofanya biashara halali katika vyumba vya biashara kwa maeneo yalioorodheshwa katika majedwali hapa chini.
2. Halmashauri ya Jiji la Arusha inapenda kuwaalika watu Binafsi, Makampuni, Ushirika, Taasisi au Vikundi vya watu vilivyojasajiliwa kisheria, wenye nia na uwezo wa kufanya biashara katika vyumba vilivyopo katika maeneo ya biashara kama ifuatavyo ;

#### **ZABUNI NAMBA LGA/003/2016-2017/M/10**

LOT. NA	ENEO	VYUMBA VYA BIASHARA	JUMLA YA VYUMBA	SIKU YA UFUNGUZI
1	SOKO KUU	ACC/SKK/01 HADI ACC/SKK/176	176	23.1.2017 Saa 4 :00 asubuhi
2	STENDI KUU	ACC/STDK/01 HADI ACC/STD 46	46	23.1.2017. Saa 4 :00 Asubuhi
3	STENDI NDOGO	ACC/STDND/1 HADI ACC/STDND/396	396	23.1.2017 .Saa 4 ::00 asubuhi
4	SOKO LA KILOMBERO	ACC/SKKLR/01 HADI ACC/SKKLR/301	301	24.1.2017. Saa 4 :00 asubuhi
5	SOKO LA KIJENGE	ACC/SKKJG/01 HADI ACC/SKKJG/103	103	24.1.2017. Saa 4 :00 asubuhi
6	SOKO LA SANAWARI	ACC/SKSNW/01 HADI ACC/SKSNW/12 NA 14	14	24.1.2017. Saa 4 :00 asubuhi
7	MGAHAWA	GREEN HURT HOTEL	01	24.1.2017.Saa 4 :00 asubuhi

8	RANGER SAFARI	RANGER /01- HADI 80	80	24.1.2017.Saa 4 :00 asubuhi
		JUMLA YA VYUMBA	1,117	

3. Mwombaji anaruhusiwa kuomba zaidi ya zabuni Moja (Chumba Kimoja) na kadri ya uwezo wake kwani kila zabuni inajitegemea.
4. Waombaji waliopo katika vyumba hivi kwa sasa wanaimizwa kuomba kwani watapewa kipaumbele iwapo watatimiza masharti ya zabuni pamoja na bei
5. Upangaji wa vyumba hivi vya biashara ni wa kupindi cha kuanzia (Aprili 2017 –Hadi Octoba 2020
6. Mpangaji wa Chumba cha Biashara atakayefanikiwa kupata chumba hataruhusiwa kumpangishia mtu mwingine (Sublets) bali kufanya Biashara yeze menyewe.
7. Zabuni zinashughulikiwa kwa utaratibu wa ushindanishi wa waombaji wenyeji Preferences to Local Community kama ilivyoainishwa Kwenye Kanuni za Manunuzi (PPA 2011) –Kanuni ya 40 .GN 446 ya 2013 Kwa hiyo iko wazi kwa waombaji wenyeji wote wa jiji la Arusha.
8. Waombaji wote wenye nia na uwezo wanaweza kupata taarifa kamili kuitia makabrasha ya zabuni katika ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni ya **Halmashauri ya Jiji la Arusha, barabara ya Boma S.L.P. 3013, Arusha**, kila siku kuanzia saa **2.30 asubuhi hadi saa 8:30 mchana**, siku za Jumatatu hadi Ijumaa [kuondoa siku za sikukuu zinazotambulika kitaifa]
9. Nyaraka za aina zote za Zabuni zitapatikana baada ya kulipa ada ya Maombi ya Tshs **50,000.(Hamsini Elfu)** Malipo ya maombi ya zabuni kufanyika kuitia akaunti ya Halmashauri ya Jiji la Arusha iliyoko katika Benki ya NMB, tawi la Clock Tower, akaunti ya Jumla **Halmashauri ya jiji Arusha. Account Na 40801200336** na kuwasilisha nakala halisi ya hati ya malipo ya Banki [Bank Pay-in Slip, original copy] na kupata stakabadhi ya Halmashauri kwa zabuni iliyoombwa. Malipo yaliyotolewa kama ada ya maombi ya zabuni hayatarejeshwa.
10. Zabuni zote zifungwe ndani ya bahasha iliyofungwa kwa lakiri [seal], na juu ya bahasha iandikwe maandishi yanayotaja **NAMBA YA ZABUNI,LOTI NAMBA YA CHUMBA, ENEO LA BIASHARA, CHUMBA NAMBA** zipelekwe katika sanduku la zabuni lililoko katika ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji kwa kutumia Anuani ifuatayo:-

**Katibu wa Bodi ya Zabuni  
Halmashauri ya Jiji,  
Barabara ya Boma,**

**S.L.P. 3013, Arusha.**

11. Halmashauri ya Jiji la Arusha hailazimiki kukubali/ kutokukubali kutoa zabuni kwa mwombaji zabuni ye yote kuto kana na kigezo cha malipo makubwa/malipo kidogo ya eneo la ukusanyaji mapato au utoaji huduma linaloombewa zabuni.

**MKURUGENZI  
HALMASHAURI YA JIJI.**